**BUNGE KUMI NA TATU- MUHULA WA NNE (2025)**
**BUNGE LA TAIFA**

# UFAFANUZI KUHUSU MSWADA WA KATIBA YA KENYA (MAREKEBISHO) (MSWADA WA BUNGE LA TAIFA NAMBARI 4 WA 2025)

## A. Je, ni utaratibu gani uliopo wa kurekebisha Katiba kwa njia ya Bunge?

1. Marekebisho ya Katiba kwa mpango wa Bunge ni pale ambapo Wabunge wanapendekeza mabadiliko kwenye Katiba.
2. Mchakato wa kurekebisha Katika kwa njia ya Bunge unaongozwa na Ibara ya 256 ya Katiba na Kanuni za Kudumu za Bunge linalohusika.
3. Ibara ya 256 ya Katiba inaeleza kwamba Mswada wa kurekebisha Katiba unaweza kuwasilishwa katika Bunge la Taifa au Seneti na utasomwa Mara ya Pili baada ya siku tisini (90) tangu tarehe ya Kusomwa Mara ya Kwanza.
4. Mswada huo utakuwa umepitishwa na Bunge pale ambapo Bunge la Taifa na pia Seneti yatakuwa yameupitisha katika hatua ya Kusomwa Mara ya Pili na Kusomwa Mara ya Tatu kwa idadi isiyopungua thuluthi mbili ya Wabunge wote wa Bunge hilo.
5. Baada ya Mswada kupitishwa na Bunge, Spika wa Bunge la Taifa na Spika wa Seneti kwa pamoja watawasilisha Mswada huo kwa Rais ili upate kibali cha Rais na kuchapishwa na wataambatisha cheti cha kuthibitisha kwamba Mswada huo umepitishwa na Bunge kwa mujibu wa Ibara ya 256 ya Katiba.
6. Pale ambapo—
   (a) Mswada haupendekezi marekebisho kwa suala ambalo linahitaji kuridhiwa kupitia kwa kura ya maamuzi, Rais, katika muda usiopita siku thelathini (30) baada ya kupitishwa na Bunge, ataidhinisha Mswada huo na kuhakikisha umechapishwa; au
   (b) Mswada unapendekeza marekebisho kwa suala ambalo linahitaji kuridhiwa kupitia kwa kura ya maamuzi, Rais—
      (i) ataagiza Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka (IEBC) kuandaa kura ya maamuzi katika muda usiopita siku tisini (90); na
      (ii) atatia kibali Mswada huo na kuhakikisha umechapishwa katika muda usiopita siku thelathini (30) baada ya mwenyekiti wa IEBC kumthibitishia Rais kwamba Mswada huo umeidhinishwa ipasavyo kupitia kwa kura ya maamuzi.

## B. Je, Mswada wa Katiba ya Kenya (Marekebisho) wa 2025 unalenga nini?

7. Lengo la Mswada huu ni kurekebisha Katiba ili kujumuisha hazina zifuatazo za umma—
   (a) Hazina ya Serikali ya Kitaifa kwa Maeneobunge ambayo lengo lake ni kuhakikisha utekelezaji wa majukumu ***mahususi*** ya serikali ya taifa katika kila eneobunge ili kuwezesha maendeleo yenye usawa kote nchini.
   (b) Hazina ya Uangalizi ya Seneti ambayo lengo lake ni kuhakikisha kwamba Seneti imewezeshwa kikamilifu kutekeleza majukumu yake ya uangalizi ambayo yanajumuisha uangalizi wa mapato yaliyotengewa serikali za kaunti.
   (c) Hazina ya Serikali ya Taifa kwa Hatua Sawazishi ambayo lengo lake ni kuimarisha mikakati ya serikali ya taifa ya kukabiliana na ukosefu wa usawa au kunyimwa kimfumo au kukiuka kwa haki au uhuru wa kimsingi.

## C. Je, Mswada wa Katiba ya Kenya (Marekebisho) wa 2025 umefikia hatua gani?

8. Mswada huu ulichapishwa kwenye *Gazeti rasmi la Serikali* mnamo tarehe 26 Februari, 2025 na kusomwa Mara ya Kwanza katika Bunge la Taifa mnamo tarehe 12 Machi, 2025.
9. Kwa mujibu wa Kanuni ya 127 ya Kanuni za Kudumu za Bunge la Taifa, Mswada huu ulikabidhiwa Kamati ya Kiidara ya Masuala ya Haki na Sheria ili kuwezesha ushirikishwaji wa umma.
10. Kamati ya Kiidara ya Masuala ya Haki na Sheria inahitajika kuzingatia maoni na mapendekezo ya umma katika ripoti yake kwa Bunge la Taifa ili kuelekeza mjadala katika hatua ya Mswada Kusomwa Mara ya Pili.

## D. Je, Kamati ya Kiidara ya Masuala ya Haki na Sheria itawezesha vipi ushirikishwaji wa umma kuhusu Mswada wa Katiba ya Kenya (Marekebisho) wa 2025?

11. Katibu wa Bunge la Taifa, kupitia kwa arifa ya tarehe 15 Machi, 2025, alialika umma na wadau kuwasilisha maoni kuhusu Mswada huu kwa Kamati ya Kiidara ya Masuala ya Haki na Sheria. Maoni hayo yanaweza kuwasilishwa moja kwa moja kwa Ofisi ya Katibu wa Bunge la Taifa; kutumwa kwa njia ya posta au kutumwa kwa njia ya baruapepe kwa Katibu wa Bunge la Taifa. Siku ya mwisho ya kuwasilisha maoni ni Jumanne, tarehe 10 Juni, 2025 saa kumi na moja jioni.
12. Isitoshe, Kamati ya Kiidara ya Masuala ya Haki na Sheria itaandaa vikao vya kupokea maoni ya umma mnamo Jumatatu tarehe 5 Mei, 2025, Jumanne tarehe 6 Mei, 2025, Jumatano tarehe 7 Mei, 2025 na Alhamisi tarehe 8 Mei, 2025 kuanzia saa mbili asubuhi hadi saa kumi na moja jioni katika Kaunti zote 47 katika sehemu mahususi za kupokea maoni zilizoorodheshwa katika arifa ya vikao vya umma.

13. Aidha, mawasilisho kwa maandishi kuhusu Mswada huu yanaweza kuwasilishwa katika sehemu mahususi za vikao vya kushirikisha umma na kwenye Ofisi za Wabunge katika Maeneobunge yote 290 ya Bunge la Taifa na Ofisi za Wawakilishi wa Kike wa Kaunti katika Kaunti zote 47, ili mawasilisho hayo yawasilishwe kwa Katibu wa Bunge la Taifa.

**E. Je, kukita katika Katiba Hazina ya Serikali ya Taifa kwa Maeneobunge, Hazina ya Uangalizi ya Seneti na Hazina ya Serikali ya Taifa kwa Hatua Sawazishi kutapunguza mgao wa fedha unaotengewa kaunti kila mwaka?**

14. Hazina ya Serikali ya Taifa kwa Maeneobunge, Hazina ya Uangalizi ya Seneti na Hazina ya Serikali ya Taifa ni hazina za serikali ya taifa na fedha zake zitatolewa kwa mgao wa fedha uliotengewa serikali ya taifa kupitia kwa Sheria ya Kugawa Mapato ya kila mwaka ambayo hupitishwa kwa mujibu wa Ibara ya 218.

15. Kwa hivyo, kuzikita Hazina hizo katika Katiba hakutapunguza kwa vyovyote mgao wa fedha kwa kaunti kwa sababu fedha hizo zitatolewa kutoka kwa mgao wa serikali ya taifa.

**F. Je, Mswada wa Katiba ya Kenya (Marekebisho) wa 2025 unaweza kurekebishwa na Bunge?**

16. Katiba imeweka utaratibu mahususi wa kushughulikia na kupitisha Miswada ya kurekebisha Katiba tofauti na utaratibu uliowekwa kwa utungaji wa sheria za kawaida. Utaratibu wa kurekebisha Katiba kwa makusudi haujumuishi michakato ya ziada kama vile upatanishi ili kuoanisha maoni tofauti kati ya Bunge la Taifa na Seneti; na Rais kutotia kibali Mswada huo baada ya kupitishwa na Bunge.
17. Maoni na mapendekezo ya umma yatatoa mwongozo kwa Wabunge ama kuidhinisha au kuukataa Mswada huu katika hatua ya Kusomwa Mara ya Pili au Kusomwa Mara ya Tatu.

***"Kwa Ustawi ya Jamii na Utawala wa Haki kwa Watu"***